



## Moyo wa mzee huendelea kuwa kijana katika mambo mawili: Katika kupenda dunia na matumaini ya muda mrefu

Imepokelewa kutoka kwa Abuu Huraira -radhi za Allah ziwe juu yake- amesema: Nilimsikia Mtume -rehema na amani ziwe juu yake- akisema: "Moyo wa mzee huendelea kuwa kijana katika mambo mawili: Katika kupenda dunia na matumaini ya muda mrefu".

[Sahih] [Imepokelewa na Al-Bukhaariy]

Ameeleza Mtume rehema na amani ziwe juu yake kuwa mzee huzeeka na mwili wake kudhoofika, lakini moyo wake huwa kijana kwa kupenda mambo mawili: La kwanza: Kuipenda dunia kwa kuwa na wingi wa mali. La pili: Kuwa na uhai na maisha na umri na matarajio ya muda mrefu.

<https://sunnah.global/hadeeth/sw/show/66221>

النّجّات الخيريّة  
ALNAJAT CHARITY



لجنة الدعوة الإلكترونية  
E-Da'wah Committee

